

Disclaimer : Ministry of Finance and Planning repository shall be regarded as a publisher and bears no liability for any damage upon using contents of the repository.

Budget Documents

Government Budget Speeches

1984-10-22

Hotuba ya Rais Mwalimu Julius K. Nyerere 1984, Semina ya Elimu Arusha

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Wizara ya Fedha

<https://repository.mof.go.tz/handle/123456789/666>

Downloaded from Ministry of Finance and Planning Repository

**Hotuba ya Rais, Mwalimu
Julius K. Nyerere**

Semina ya Elimu

Arusha : Tarehe 22 Oktoba, 1984

HOTUBA YA RAIS NYERERE KWENYE SEMINA YA ELEMU ARUSHA: OKTOBA 22, 1984

**Ndugu Waziri, Ndugu Walimu, Waheshimiwa Wageni
wetu na Marafiki zetu.**

Katika Semina hii mtajadili Sera ya Elimu katika Tanzania na utekelezaji wake; na kwa sababu hiyo mtakuwa mwikijadili batima ya nchi yetu. Jambo hiyo ni muhimu na limefikiriwa kwa wakati unaofaa. Maana kujitapa kwetu kwa mafanikio yetu ya elimu tangu tujitawale mara nyingi hakulingani na ukweli ulivyo; na hiyo ni hatari.

Tunazo sababu za kweli za kujivunia. Tumefuta ujinga wa watu wazima kwa kiasi kikubwa, na tumepanua shule zetu za msingi kiasi kwamba karibu watoto wetu wote wanakwenda shule wafikapo umri wa miaka saba; idadi ya vijana wetu wanaoingia katika shule za sekondari na katika vyuo vya elimu imeongezeka sana kuzidi bali ilivyokuwako wakati wa kujitawala, au bata mwaka 1967.

Lakini mafanikio hayo hayatoshi. Tunapaswa kutazama tena ubora wa elimu tunayoitoa, na hasa kuipima kama inalingana na mahitaji ya Tanzania. Maana ingawa baadhi ya shule zetu na vyuo vingine vya elimu ni vizuri sana, ukweli ni kwamba, kwa jumla, tumekuwa hatufanyi yale tuliyokusudia. Vile vile iko hatari kwamba tusipojichunguza upya na kujisahibisha, elimu tunayoitoa itaendelea kuongezeka katika mkondo tofauti kabisa na ule tuliokuwa na kujitawala, kwa maendeleo ya Tanzania katika uhuru na usawa.

Kujichunguza buko na maandalizi hayo ndiyo shabaha ya Semina hii. Ili na mimi niweze kusaidia katika kujichunguza buko, maneno yangu mengine yatakosoa baadhi ya mambo ambayo tumekuwa tunafanya, na utaratibu wetu wa kuyatenda mambo hayo. Kwa hiyo ningependa sasa, mapema kabisa, nitamke shukurani zetu na deni kubwa la Taifa hili kwa walimu wetu wa Shule za Msingi, Shule za Sekondari, Vyuo vyetu na Vyuo Vikuu.

Walimu wetu wako kila mahali; wako katika viji ni vyetu vyote na katika miji yetu yote. Misbahara yao ni midogo, hali zao za maisha na za kazi ni ngumu sana, na kazi wanazotakiwa kuzifanya ni nyingi mno. Nimelazimika mara nyingi kuwashawishi bila mafanikio wataaluma wengine wajaribu kujihusisha na maisha ya wananchi wanaowahudumia na kuishi nao. Walimu wa shule, na hasa walimu wa shule za msingi, hawabitaji kushawishiwa. Wengi wao ndivyo wanavyofanya. Kwa niaba ya Chama na Serikali napenda kuwapongeza walimu wa Tanzania kwa kazi na imani yao. Ni wajibu wetu wote kuendelea kuwasaidia na kuwatiamoyo.

Lakini katika taratibu zetu za jadi, suala la elimu lilikuwa suala la jamii nzima, na liliwahusu watu wote; walikuwako tu ~~watalamu~~ kwa maana ya kwamba watu fulani walitambuliwa kuwa wanajua zaidi au ni hodari zaidi wa kutendajambo maalum. Siku hizi tunao utaratibu maalum wa kufundisha vijana wetu katika shule na vyuo. Na kwa ajili hiyo tumeanza kufikiri kwamba elimu maana yake ni mafunzo yale tu yanayotolewa darasani, yanayopangwa na kudhibitiwa na shule zilizoanzishwa kwa mujibu wa sheria. Na tunajaribu kujenga ukuta wa kuzingira taratibu hizo, kwa kuamini kwamba wale tu waliomo ndani ya ukuta huo ndio wanaojua nini cha kufundisha, na namna ya kufundisha, na pengine hata nani wa kumfundisha.

Kwa kiwango ambacho tumekubali kutumbukia katika mtego huu, tumeitenga elimu ya Tanzania na jamii ya ~~Watanzania~~, na tumeifanya elimu hiyo ishindwe kutosheleza matazamio ya ~~Watanzania~~. Walimu wa kweli na watu walio hodari katika mipango ya elimu, kwa sababu ya utaalamu wao, ni wale wanaojitabidi wakati wote kuwashii kisha watu wengine katika kazi ya kuelimisha na kufundisha, wakitumia utaalamu wa watu wengine. Watatafuta kila njia ya kuoanisha elimu na maisha ya Mtanzania hapo alipo, vijijini mwetu, na mijini mwetu, katika mazingira mbali mbali.

Hayo ndiyo mambo ya msingi niliyojaribu kusisitiza miaka 17 iliyopita katika kijitabu kile **Elimu ya Kujitegemea**. Siku moja mkutano wa hadhara ulishangaa sana niliposoma

tu Azimio la Arusha badala ya kutoa hotuba kama kawaida. Kwa hofu hiyo ya kuushangaza mkutano huu sikusudii kuwasonea yale niliyoyaandika mwaka 1967. Lakini sijui ni wengapi kati yenu walijiandaa kushiriki katika semina hii kwa kusoma tena Elimu ya Kujitegemea, na kufikiria maelekezo yaliyosemwa mle pamoja na uzoefu tuhioupata katika kipindi cha miaka 17 iliyopita. Kama hamjasoma nawashauri nifanye hivyo.

Maana kijitabu kile kilifanua shabaha ya elimu kikaeleza kwa muhtasari aina ya jamii tunayojaribu kuijenga, na kuelekeza kazi za shule zetu. Kilieleza kwamba iko haja ya kuelekeza elimu ya msingi katika kuwaandaa wauafunzi waweze kuishi maisha ambayo vijana walio wengi wataishi, na elimu ya sekondari iwe elimu ya "huduma kwa wengi". Kilielekeza shulee za misingi zifanywe kuwa nisehemu ya maisha ya kijiji, zikipanga mihula yao na ratiba za masomo, na vile vile namna ya mafunzo yenyewe, katika namna itakayowawezesha wanafunzi kushiriki katika kazi za kijijini. Na kimesema kuwa kila shule ya sekondari iwe na shamba au kiwauda kidogo ambacho wanafunzi wangeweza kulekumia kuzalisha mali, na huku wakijifunza wakati wakifanya kazi.

Sina hakika kama tunaweza kusema, kwa dhati kabisa, kwamba kweli mambo hayo yanatendeka; kila mahali, au hata katika sehemu nyingi. Baadhi ya shule zetu, pengine shule nyingi, zinajaribu. Nasikia kwamba katika sehemu nyingi za Mkoa wa Tanga baadhi ya vipindi katika shule za misingi hutumikaa kwa kazi zinazolingana na mahitaji ya kijiji chao au tarafa yao, katika mpango unaoitwa "Elimu ya Vitendo". Nasikia kwamba mpango huo tayari unaleta manufaa katika maendeleo ya kilimo katika sehemu hizo. Na kwa kweli katika shule zilizoshirikishwa vema katika shughuli za kijiji hatupata malalamiko mengi juu ya kukosekana kwa vyombo au vifaa vya kufundishia, ukiacha vitabu uakaratasi; maana kupata vifaa au zana hizo ni sehemu ya mafunzo yenyewe, na halafu vifaa hivyo hutumikakatika mada rasa mengine pia.

Na ziko shule fulani za sekondari (kama vile Weruweru, Rungwe, Ruvu, Ilboru, pamoja na Nangwa) zinazotoa mazao na kuyatumia, na hivyo zina weza kuchangia gharama za maendeleo yao kwa kiasi kikubwa. Na inaelekeza kuwa katika sbule za sekondari kama hizo kuna ubusiano mwakubwa kati ya kujitegemea, uwezo wa masomo, nifhamu ya shule, na kuchangamka kwa wanafunzi na walimu. Si kweli kwamba shughuli za kujitegemea zina athari mbaya kwa masomo ya darasaani. Badala ya kuwa na madha ra kwa mafuriko ya sayansi, shughuli za kujitegemea zilizopangwa na kuoanishwa vizuri (ziwe ndani ya shule au sehemu ya juhudi ya kijiji) huwa ni za msaada kwa masomo hayo. Hupunguza tabia ya kufundisha kwa kuhtutubia wanafunzi, na kuendeleza tabia ya kufundisha kwa kuona, kwa kushika na kutenda.

Ziko shule nyingine vile vile ambako walimu wake wakuu wanajaribu kufuata mwelekeo huo. Lakini ukweli ni kwamba muundo na taratibu zetu za elimu, na vile vile wakati mwingine msukumo na malalamiko kutoka katika jamii na katika Chama, hayakusaidia mwelekeo huo; badaa yake yameuharibu. Kwa mfano: tunapanga mihula ya shule na vipindi vyatichini na zima katika Wizara, Dar es-Salaam; lakin majira ya kilimo, ua mahitaji ya mazao mbali mbali, ni tofauti katika kila Wilaya. Wazazi kijijini watapaataje msaada wa watoto wao wa shule za msingi katika kazi kubwa ya kucbuma pamba au kahawa? Hata kama shule ina shamba, kama sehemu ya shamba la kijiji, wanafunzi hawawezi kupata nafasi ya kufanya kazi inayotakiwa kufanywakatika shamba bilo kwa wakati wake, kama mpangilio wa vipindi hautoi nafasi hiyo. Au, vile vile, tunazitaka shule zishinkj pamoja na wananchi wengine katika jamii kujenga nyumba za walimu. Lakini wakifanya hivyo kodi ya nyumba inakwenza katika Mapato ya Serikali Kuu au ya Wilaya. Shule hata haziwezi kuwa na mfuko wa kuzitunza nyumba hizo au kuzijenga ziwapokuwa zimechakaa.

Kwa mujibu wa sheria tunao utaratibu wa kuwa na Bodi za Shule na Kamati za Shule za Msingi. Lakini madaraka yake ni madogo; mara nyingi Kamati hizo

hazikutani kama inavyotakiwa, na kauli ya Kamati juu ya mambo yanayotokea shulenii ni ndogo sana. Zaidi ya hapo batufanyi juhudii maalum ya kuwashirikisha wazazi katika mambo yanayofanywa na shule. Ni jambo la kawaida kabisa katika nchi zilizoendelea kuwa na vyama vinavyowaunganisha Wazazi na Walimu; lakinii katika Tanzania ni kitu cha nadra kwa shule hata kuwa na siku ya **Wazazi**, achilia mbali kuchukua hatua za kuna msaada wa wazazi katika kuifanya kazi ya shule ilingane na maisha ya Tanzania, au katika shughuli ~~ma~~ maendeleo au katika matatizo ya nidhamu.

Ukweli ni kwamba ~~matib~~ zetu za shule hazitoi elimu ya kujitegemea; bado shule zetu zinaendeshwa kana kwamba fedha za kugharimia elimu hiyo si tatizo linallowabu wanafunzi, na kana kwamba kila mmoja wa wanafunzi hao ana kazi ofisini au kiwandani inayomongoja mara atakapomaliza masomo yake. Kijana anapomaliza elimu tunayompa, uwezo wake wa kujitegemea na wa kuchangia katika uzalishaji mali mara nyingi ni mdogo zaidi ukilinganisha na mwanafunzi aliyekuwa amemaliza kipindi kama hicho katika shule ya Mkoloni. Kwa mfano, wakati ule wanafunzi walikuwawakifundishwa jinsi ya kutengeneza na kutumia mboji na samadi, au jinsi ya kuwatengenezea kibanda sungura, au kujenga ukuta, n.k.; waliyafanya mambo hayo kama sehemu ya maisha yao ya shulenii. Shule ya Sekondari ya Malangali na Shule ya Walimu ya Mpwapwa zilikuwa ni miongoni mwa shule zilizokuwa na sifa nzuri sa na ya shughuli za kujitegemea. Lakiui hazikuwa shule peke yake zenye shughuli hizo. Sasa mambo hayo yamefanywa kuwa ni "somo" tu la darasani, ua mara nyingi tunaamua kuwa batuna muda wala vifaa vya kuzitendea kazi hizo, au tunadharau kazi hizo kwa kuwa matokeo yake bayatakuwa mazuri kama yale ya kazi za mafundi stadi.

Yafaa tulitazame tena suala zima la elimu, na tulitazame katika bali halisi ya Tanzania; maisha yalivyo, na uchunii ulivyo.

Msingi ambao ni lazima tuijenge ni elimu inayoweza kusaidia na iliyo sehemu ya jamii yetu ya sasa na ya baadaye. Na lazima tuanze hatua hiyo hivi sasa; maada kama

tukijaribu kuendelea na utaratibu wetu wa sasa, na hali yetu ya uchumi ikiwa hivi ilivvo, basi hata kima cha elimu tunayoitoa hivi sasa kitadidimia. Kwa sababu zilizo nje ya uwezo wetu pato la Taifa limepungua. Nakwa sababu hatuna uwezo wa kuagiza kutoka nchi ~~za~~ nje bidhaa nyingi tulizozoea kuagizahuko nyuma, tundalazimika amakuongeza mazao yetu wenyewe na kuyatumia hayo tunayoyazalisha, ama kuwa na rasilmali pungufu zaidi za kutumia katika elimu na huduma nyingine.

Tuna haja pia ya kuliaugalia suala hilo katika sura ya matumaini yetu ya kuleta Maeudeleo ya Kijamaa. Nime-pata kuwaambia wanajeshi wetu kwamba nchi haiwezi kujenga ujamaa ikiwa jeshi lake haliko tayari kujenga na ku Linda ujamaa. Lakini labda ni kweli zaidi kusema kuwa nchi haiwezi kujenga ujamaa ~~ikiwa~~ waalimu wake hawakubali kujenga ujamaa; ikiwa elimu yake si elimu ya kujenga msingi na tabia ya kijamaa na ya kujitegemea. Mtoto umleavyo ~~ndivyo~~ akuavyo.

Katika kuichambua tena elimu yetu, jambo la **kwanza** ambalo hatuna budi kulikubali ni kwamba maendeleo ya baadaye ya Tanzania na watu wake wote ~~yata~~ tegemea **elimu ya msingi**. Hilo ndilo tegemeo la maisha ya baadaye ya watu wetu. Hiyo ndiyo haki ya raia wote; na wengi wao hawatapata elimu zaidi ya darasani baada ya kumaliza elimu ya msingi. Kwa hiyo iko haja ya elimu ya msingi kuwa elinu nzuri, elimu inayotosheleza, na elimu inayolangana na uwezo wa **wanafunzi** kuwa raia watakaozalisha mall na watakaoshiriki kwa ukamilifu katika maendeleo ya **nchihuru** na inayojenga ujamaa.

Elimu ya msingi haina budi iwapatie **wanafunzi** wetu msingi mzuri wa kusoma, kuandika na kuhesabu. Haina budi iwavezeshe kujua Kiswahili vizuri na kujenga msingi mzuri wa Kiingereza. Miaka saba inatosha kabisa kuyakamilisha yote haya. Elimu ya msingi ingepaswa pia kufundisha historia na utamaduni wa Taifa letu na wa Afrika. Hii ~~itaj~~ nsaidia **mwanafunzi** kuongeza ujuzi wake wa utamaduni wetu na historia yetu ambao alikuwa amepata kutoka kwa wazazi wake. Elimu ya msingi ingepaswa kuwasaidia vijana kupenda kuwa wadadisi, na kujenga fikira

za kisayansi, yaani udadisi katika taratibu za kutenda mambo, kwa msingi wa kujua rasilmali zilizopo pale pale walipo na katika Taifa lao. Katika hatua za mafunzo ya aina hiyo Elimu ya Msingi inapaswa impatie mwanafunzi ufundi na maarifa yatakayomsaidia baadaye kuishi maisha bora vijiji au mijini mwetu.

Kama vile kilimo ndicho uti wa mgongo wa ucbumi wetu, basi Elimu ya Msingi ndiyo nguzo na msingi kweli wa maendeleo yetu yote. Haikuitwa Ellmu ya Msingi bure. Ndiyo Elimu ya Wote. Ndiyo Elimu Kuu ya Taifa letu. Kwa sasa inachukua miaka saba. Uwezo wetu utakapo-ongezeka, itachukua muda mrefu zaidi. Kwa hiyo kazi yetu ya umuhimu wa kwanza katika elimu ni kuongeza ubora wa Elimu ya Msingi na kuipanua ili ikidhi mahitaji hayo niliyye yaeleza, na ilingane na ongezeko la watu. Ingepasa, baada ya elimu ya msingi, kijana awe na uwezo na mwelekeo wa kutoa mchango wake kwa jamii wakati ule ule anapoendelea kujifunza kutoka katika jamii hiyo.

Na kama elimu yetu ingekuwa kweli ni Elimu ya Kujitegemea, mabadiliko ya kijana kutoka katika maisha ya shule na kuingia katika maisha ya kijijini yangekuwa rahisi na jambo la kawaida; maana shule ingekuwa ni sehemu ya kijiji katika uzalishaji mali, katika elimu na katika maisha ya jamii. Maana Shule ya Msingi ni shule ya jamii. Huko nyuma tumejaribu kuanzisha Shule za Jamii ili ziwemifano ya shule zetu zote za msingi. Badala ya vyombo vyetu vya elimu kufikiria shule hizo kuwa shule za ovyo zenye mipango migumu inayolazimishwa na wanasiasa, na bivyo kupingwa na kusukumiwa katika mitindo ile ya awali, vyombo hivyo vinjepaswa kuziona shule hizo kuwa ni vielelezo vya kuigwa na shule zote za msingi. Shule ya Msingi isipokuwa shule ya jamii, itakuwa shule ya nini? Ni kwa kuwa shule ya jamii ndipo inapoweza kutimiza shabaha yake ya kujenga jamii ya kesho.

Na kwa Taifa letu umuhimu wa pili kwa Elimu ya Msingi ni Elimu ya Watu Wazima na Elimu ya Ufundi. Hii nayo haina budi ipangwe kwa namna itakayowasaidia watu kuinua hali ya maisha yao, na wala isielekezwe kauntka kupata yeti vya elimu ya sekondari. Lazima mka zo uwe

katika kuongeza utaalamu, hasa utaalamu wa klimo, lakini si klimo peke yake. Wananchi wanafahamu mabitaji yao. Waulizeni! Wakisha kuwambia, waandalieni mafunzo yao. Walimu wapo, mijini na vijijini. Maana pamoja na walimu wa shulen, wapo pia katika au karibu na kila kijiji, angalau Bwana Shamba mmoja, au Mhasibu, au Seremala, au Fundi Mitambo, au mtu mwenye ufundi mwingine. Siku zote katika historia watu wamekuwa wakifundisha bila ya wao wenyewe kupata mafunzo ya ualimu, na katika masomo ya watu wazima na ya ufundi hatujaendelea kiasi cha kuweza kuwa wataaradhi sana juu ya walimu!

Baada ya mafanikio makubwa tuliyoyapata katika kupunguza ujinga, hatuwezi kulegeza jiti hada zetu katika elimu ya watu wazima hivi sasa, eti kwa sababu tu nchi yetu ni maskini. Maendeleo hayo ni mwanzo tu, siyo mwisho. Tusi poufuta ujingga tutaendelea kuwa maskini.

Na mafunzo ya teknolojia kwa vijana wetu ni muhimu kwa maendeleo yetu ya siku za mbele. Kupanuka kwa elimu ya msingi lazima kuambatan e na juhud i zetu za kuinua elimu ya ufundi. Tunaishi katika dunia ya teknolojia. Kinachoturudisha nyuma katika maendeleo ya taifa letu ni ujingga wetu, na basa ujingga wetu katika mambo ya ufundi na teknolojia. Maana yake ni kwamba hatujifan yii wenyewe kazi ambazo zingeweza kufanya kwa urahisi kwa kutumia rasilimali zetu, kama watu wetu wangekuwa na uwezo mkubwa zaidi wa ufundi; na maana yake pia ni kwamba tunaharibu mashini tunazoziagiza kutoka tje, na wala batuna uwezo wa kununua mpya. Hatuwezi kutengeneza zana zetu wenyewe, na hizo tunazoagiza hatuwezi kuzitunza. Huu ndio upungufu wetu wa kwanza. Kazi kubwa ya elimu yetu nikuu ondoa au angalau kuupunguza.

Tumetamka shabaha ya kujenga shule za ufundi katika Wilaya; lakini ni shule chache sana za namna hiyo ambazo hivi sasa zinafanya kazi. Liko tatizo la kuagiza vifaa na mitambo, lakini tumeruhusu tatizo hili lituvunj je moyo. Lazima tuenze hapa hapa tulipo. Kama batuna kerezo, tuenze na msumeni. Tumi a zana iliyopo, na kueneza ujuzi ambao watu wetu wachache wanao. Heri hivyo kuliko kukosa kabisa, ambayo ndiyo hali ya sasa. Angalau

kufanya hivyo kutawafanya vijana wetu wazoe kazi, na kudumisha katika jamii yetu ujuzi fulani ambao wazee wetu walikuwa nao. Kwa kweli kuanza na zana za asili kunaweza kusaidia kuifanya elimu yetu ya ufundi kuwa elimu ya vitendo hasa. Tukipata uwezo zaidi tunaweza kuongeza vifaa vipyta na walimu waliofunzwa vizuui zaidi. Lakini mara nyingi si umasikini unaofanya tukose kerezo. Mara nyingi hatuna randa au kerezo kwa sababu hatuipi umuhimu elimu ya ufundi. Mbona magari tunayo?

Baada ya kuzungumza juu ya Elimu ya Msingi, na Elimu ya Ufundu na ya Watu Wazima, sasa nafkia suala linalonekana kuwa linapendwa sana na wataalamu wa elimu na wanasiasa pia: yaani Elimu ya Sekondari. Ni dhahiri kwamba hatuua budi tupanue elimu ya sekondari. Lakini ni vizuui sababu za kweli za kupanua elimu ya sekondari zikaelekewa. Elimu ya Sekondari haiwezi ikawa ni elimu ya Watanzania wote. Tunalazimika kupanua elimu ya sekondarikwa sababu hatuwezi kupanua au kuinua kiwango cha elimu yetu ya msingi na ya ufundi bila ya kupata walimu walioopata Elimu ya Sekondari. Kadhalika ziko buduma mbali mbali ambazo zitahitaji zitolewena watu ambao elimu yao inazidi miaka saba. Kwa siku za mbele tunazoweza kuzifikiria hiyo ndiyo shabaha ya elimu yetu ya Sekondari, yaani kupata watu tunaoweza kuwfundisha kuwa Walini, Mabwana-shamba, Madaktari, Mafundi, na kadhalika. Hatuna sababu nyingine ya kutoa Elimu ya Sekondari; maana Elimu ya Sekondari si haki ya kila Mtanzania kama vile ilivyo Elimu ya Msingi.

Natambua kuzamha kazihi maledamiko yote ya kitalaka ongezeko la elimu huja katika sura ya kudai Shule za Sekondari zaidi. Na shule za sekondari zinazopendwa kupita zote ni zile ambazo Waingereza walikuwa wakiziita "Shule za Sarufi". Kwao shule hizi zilikuwa ni shule za watoto wa tabaka ya watawala Mamwinyi wa Kiingereza. Kwao shule hizi zilikuwa zikifundisha Kiingereza, Kilatini, Kigiriki na Ubwana. Walipoanza kuzijenga hukukwetu zilikuwa zinakusudiwa hasa kwa watoto wa machifu. Mara nyingi tunapodai sana elimu ya sekondari, tunachodai siyo elimu

yen yewe, lakini "ubwana" unaotazamiwa k u tokana na elimu hiyo. Nasema kwamba ni jukumu la Chama na Senkali, na hasa Wizara ya Elimu, kuzuia mwelekeo huo.

Tumetanga za kuwa tuna taka kuongeza nafasi za masomo ya sekondari, na kufanya hivyo zaidi kwa msingi wa kuanzisha shule zisizok uwa za bweni ili kupunguza gharama. Vile vile tumetangaza kuwa wale watakaokwenda katika shule za sekondari za bweni, watalipa ada ili wachangie kidogo gharama za chakula na malazi. Sina tatizo na maamuzi hayo, na wa la sisemi kuwa tuyabatilishe. Lakini maamuzi hayo hayatoi jibu la tatizo la kutoa elimu nzuri ama ya Msingi aina ya Sekondari; na vile vile ni maamuzi yanayoweza kuzaa matatizo muengine. Kama tunataka kudumisha haki sawa kwa vijana wetu wote, itakuwa lazima i wcko aina filani ya misaada k wa watoto wa wazazi ambao k wa k welihawawezi kumudu gharahazo. Matumaini yangu ni kuwa Serikali za vijiji na Serikali za mitaa zitatoa misaada hiyo k wa wazazi ambao hawana uwezo kabisa. Na kama tunataka kutetea usawa wa haki za mtoto wa kijijii, lazima vile vile tushughulikie suala la mahali pa kukaa, na jinsi atakavyotunzwa k wa uangalifu na nihamu, ikiwa shule yen yewe ya siku haiko karibu na Kijiji chake.

Kazi yetu ni kupanua elimu ya sekondari wakati walimu na angalau vifaa muhimu vinapatikana; laki ni siyo kabla ya hapo. Maa na batuwezi kupanua elimu ya sekondari, bila walimu na bila vifaa. Kujaribu kufanya hivyo ni kuwadanga nya wananchi. Tutakuwa tunawapa wauanchi kitu ambacho tunakiita Elimu ya Sekondari na kuwatoza ada, na kumbek wa k weli si elimu ya sekondari. Tutakuwa walanguzi wa elimu! Na hayo yanahusu shule za serikali na za watu binafsi. Hivi sasa shule zetu nyingi za sekondari, na hasa shule za binafsi, (lakinisihizo peke yake) zinawalaghai wananchi. Hazifa nyi hivyo k wa nia mbaya, ila k wa sababu hazi na walimu, wala vitabu, wala vifaa (hasa vya masomo ya sayansi) ambavyo ni vya lazim a ikiwa elimu ya kweli ya sekondari itatolewa. Huwa tunasema k wa haraka sana kuwa majengo yata patikana k wa uwezo wa wanaanchi wen yewe. Lakini majengo si muhimu sana. Kama mfano wa shule ya Nangwa unavyoonyesha,

baada ya kuweka msingi kidogo tu, majengo ya kawaida yanawenza knjengwa kwa jubi za pamoja za wanafunzi na walimu, ikiwa ni sehemu ya kujifunza na kufanya kazi hapo hapo katika shule. Jambo la muhimu katika Elimu ni walimu na vitabu, na; katika masomo ya sayansi, maabara. Ukiacha maktaba na maabara, majengo yanawenza yakawa mabanda ya kawaida tu, kama walimu na wanafunzi wananuia kweli kusoma. Lakini ni vizuri kusisitiza pia kwamba shule zetu za msingi nyingi bado zina upuugufu mkubwa wa madarasa na nyumba za walimu. Kama tuna uwezo wa ku jenga ni vizuri tuzisaidie kuondoa upungufu huo.

Bado liko jambo moja linalopaswa kntiliwa mkazo. Po pote, na wakati wo wote tuna poanzisha shule ya sekondari, lazima shule hiyo iwe ni shule ya sekondari ya ufundi: nyingi zitakuwa na mchepuo wa kilimo na inasino mengine ya sayansi. Mtu mwenye elimu ya sekondari ya mchepuo wa sayansi au kilimo anaweza kufundwa kazi za uendeshaji, kama ni lazima. Tunao waendeshaji wa Idara mbali mbali ambao ni wataalam wa taaluma fulani. Lakini mtaalamu wa mambo ya uendeshaji hawezi kuwa Bwana Shamba, au Mbandisi. Mimi siwezi kuwa Mbandisi, la kini Mbandisi anaweza kuamua kuwa Mwalimu au Mwanasia sa!

Kama vile ambavyo kuinirisha na kupanua Elimu ya Msingi kunabitaji kupanua na kuongeza shule za sekondari, kadhalika elimu ya msingi na ya sekondari zina hitaji kupanua uwezo wa kufundisha walimu. Ile mipango mingine yote haitafaulukamahatuliti sua la bili inkazo wa kutosha. Maana tunabitaji walimu zaidi, na walimu oora zaidi; yaani, tunabitaji idadi kubwa zaidi ya walimu wapya, na walimu waliopo wapate mafunzo zaidi katika kazi zao. Tunaeendelea kuzungumza juu ya kupanua mafunzo; la kini ukweli ni kwamba tuna upungufu mkubwa sana wa walimu. Hivi sasa tunao asilimia 75 tu ya walimu wa shule za msingi tunafahamu kuwa wanabitaji kwa madarasa ya wanafunzi hamsini: na hilo ni darasa kubwa mno kwa mwalimu kufundisha vizuri. Vile vile tuna asilimia 73 tu za nafasi za walimu wa sekondari zilizojazwa: na kwa masomo mengine (kama masomo ya ufundi) nafasi zilizo wazi ni

nyingi zaidi. Shule za msingi zinakadiriiwa kuwa na upungufu wa walimu 24,000, na shule za sekondari upungufu wa walimu 875. Hata Vyuo vya Elimu vina asilimia 20 ya nafasi zao wazi, au upungufu wa walimu 300. Aladi yetu ya elimu kwa watoto wote waliofikia umri wa kusoma, na mipango yetu ya kuanzisha shule mpya za sekondari, haitakuwa na maana yo yote kama hatukutua tafizo la upungufu wa walimu.

Katika Vyuo vya Elimu vyenyewe, lazima tufanye juhudini ya makusudi kuelekeza mafunzo kwenye masomo ya ufundi. Na hasa batuna budi kujenga katika mawazo ya wakufunzi uwezo wa kubuu mbinu mpya za kufundisha, na kutumia kwa vielelezo vifaa vyovytote vinavyoweza kupatikana hapo watakapopangiwa kufundisha. Na lazima wasaidiwe kutambua manufaa ya kufuta ushirikiano wa wananchi wanaoishi katika eneo lao, ambao wana ujuzi maalum wa eneo hilo au wa ufundi, katika kujifunza wao wenyewe na wanafunzi wao.

Sehemu kubwa sana ya elimu katika nchi hii hivi sasa inatolewa, na itaendelea kutolewa, na Serikali Kuu au Setikali za Mitaa. Lakini rasimili zetu ni kidogo mnaji kuweza kutimiza yote yanayohitajiwa, hata katika maeneo tunayoyatilia umuhimu wa kwanza wa Elimu ya Msingi, Elimu ya Ufundi na Elimu ya Watu Wazima. Na hasa tunayashukuru mashirika ya kujitolea kwa ajili ya kujenga na kuendesha shule zetu nyingi za watoto walemavu, na napenda kuyapongeza kwa kazi inayofanywa. Wakati huo huo lazima tutambue kwamba, kwa kadiri inavyoweza kana ni vizuri sana watoto hawa walemavu waingizwe katika shule za kawaida, wasome pamoja na wenzao. Hiyo imekuwa ndiyo sera yetu, na imeendelea kuwa sera yetu. Lakini inaviongezca kazi Vyuo vyetu vya Walimu. Maana walimu wetu lazima wafahamu kwamba wanawenza kuhitajika kutoa nisaada maalum kwa mtoto mwenye upungufu, au mwenye matatizo ya kusikia, au kuona vizuri, au ambaye ana matatizo ya kutumia kiungo fulani cha mwili wake. La muhimu zaidi ni kwamba watapaswa kuwatia moyo watoto na wanafunzi wengine kuwakubali watoto walemavu hao na kuwa nao kama kawaiða, na kuwasaidia inapokuwa lazina.

Ndugu WaJimu, lazima elimu yetu iwave ufundi watu wetu: watoto, vijana na watu wazima. Lazima vile vile isaidie kujenga hisia zinazofanana na maendeleo ya nchi yetu. Kwa sasa bado tunahangaika na tatizo kwa sababu watu wetu hui fikiria elimu ya shule kuwa ni mafunzo ya kufanya kazi mijini. Na mara anapomaliza masomo, hasa kama amemaliza shule ya Sekondari au Chuo Kikuu, anatarajiwa kuondoka kijiji. Matokeo yake ni kwamba vijana wetu wasomi wanakuwa ni wakimbizi katika nchi yao wenyewe. Wanayakimbia maisha ya mazingira yao, badala ya kutaka kuyabadili. Hii ni dalili na kipimo cha kasoro katika elimu yetu. Maana watu wetu wanaishi na kufanya kazi vijiji; na huko ndiko kwenye manufaa ya nchi yetu. Tunakimbia kwenda wapi?

Hasa kuna wazo moja ambalo lazina tulipige vita, nadhani tuenze na sisi wenyewe. Ni wazo kwamba mtoto asipochaguliwa kuingia katika shule ya sekondari basi ameshindwa. Ameshindwa nini? Elimu ya msingi ni ya miaka saba. Mwanafunzi akiikanilisha, basi, aine-*i*ka*ni*lisha: amefaulu. Wachache tu miongoni mwao watachaguliwa kwenda kidato cha kwanza. Wengi ne hawatachaguliwa. Na hawatachaguliwa siyo kwa sababu wameshindwa cho chote, lakini kwa sababu nafasi za kidato cha kwanza ui chache. Kama kuna kushindwa, basi, ni Serikali na Nchi kwa jumla ili yoshindwa kufanya elimu ya Sekondari iwe ni kwa wote. Katika hali yetu ya sasa tunajua kuwa hata kama wanafunzi wetu wote wanaomaliza darasa la saba wangeshinda matihani wao mia kwa mia, idadi ambayo ingechaguliwa kuingia katika kidato cha kwanza ingebacki ni ile ile. Maana kutopata nafasi katika shule za sekondari hakutokani na akili za watoto hawa kuwa ni duni, bali kunatokana na uchumi wa nchi yetu kuwa ni duni.

Lakini mawazo haya tunaendelea kuwa nayo kwa sababu tunakataa kukubali shabaha ya kweli ya elimu ya msingi. Tunaendelea kuamini na kujidanganya kuwa shabaha ya elimu ya msingi ni kutayarisha wanafunzi kupata elimu ya sekondari. Kwa hiyo basi kijana ye yote asiye pata nafasi katika Shule ya Sekondari kashindwa. Tungekubali tangu mwanzo kwamba shabaha ya elimu ya msingi ni kuwa andaa

vijana wetu kwa maisha ya baadaye, baada ya elimu ya msingi, basi tungewaandaa kwa niaisha hayo: mtihani wao wa kweli ungekuwa ni mtihani wa niaisha hayo. Anayefaulu aukushindwa angefaulu au kushindwa katika maisha hayo. Tusingekuwa tukiwakejeli vijana wetu na Taifa la kesho kwa kuwaandaa kwa mtihani wa kuingia katika shule za sekondari ambazo tuna jua kuwa hazipo.

Kama hatukisfaniki wa kulishinda wazo hili mapema, tutaanza kuamini kwamba Taifa letu ni Taifa la watu walioshindwa: taifa la watu punguani watupu, isipokuwa wale wachache waliowahi kupata Elimu ya Sekondari. Lazima niilani kabisa tabia hii maana namua moja ya watu wachache wenye bahati au uwezo fulani kujenga hali ya unyonge kwa walio wengi ili waendelee kuwanyanya na kuwanyonya kama kwamba hawana akili. Maana sasa hivi watoto wanaoingia katika Shule za Sekondari baada ya kumaliza Elimu ya Msingi ni kiasi cha asilimia 2 tu, na hakuna matarajio ya kiasi hicho kuongezeka sana katika miaka ya karibuni. Wala hakina sababu ya kuongezeka. Tutakapopata uwezo zaidi wa kuongeza huduma zetu za elimu, tutapaswa kupunguza idadi ya watoto wanaosoma katika darasa moja na kuongeza miaka ya kusoma katika Shule ya Msingi, ili tuweze kuinua kiwango cha elimu ya ufundi. Sasa hivi tunawaelimisha watu kutamani maisha bora, lakini hatuwafundishi jinsi ya kujenga maisha bora.

Hiyo ndiyo kazi kubwa iliyoko mbele yetu; na kazi hii lazima tufanye japokuwa uwezo ni mdogo na rasilimali zetu zinazidi kupungua. Kwa hiyo hatuna budi kupanga mambo yetu kwa umuhimu wake, na kuleta maendeleo yetu kwa kufuata bila kubabaika umuhimu wa inipango hiyo. Mambo yote tuliyosema kwamba tunataka kuyafanya, hata yale tuliyosema tunanuia kuyafanya, yote ni mambo mazuri. Lakini hakuna uwezekano wa kuyatenda yote hivi karibuni. Kama tukijaribu kuyatekeleza yote kwa mara moja elimu yetu nayo itafanana na majengo mengi ambayo yameanzishwa na kuachwa bila kukamilishwa na hakuna lo lote la maana linalofanyika. Umuhimu wetu wa kwanza ni Elimu ya Msingi nzuri na inayofaa kwa vijana wetu wote. Umuhimu unaofuata ni Elimu ya Ufundi na Elimu ya Watu

Wazima. Shabaha kubwa ya maeneo yaliyo baki ni kuya-wezesha maeneo hayo kuhudunia Elimu ya Msingi, Elimu ya Ufundu, na Elimu ya Watu Wazima, kwa gbarama ndogo kadiri inavyowezekana.

Na hasa uendeshaji katika mambo ya elimu lazima ufanywe kwa ufanisi, na kwa kutumia rasilmali kidogo kadiri inavyowezekana. Mimi sidhani kuwa hivyo ndivyo ilivyo hivi sasa. Haiwezekani kuwa elinisha Watanza nia milioni 20 kutoka Dar es Salaam. Makao Makuu ya Wizara ya Elimu ya da weza kuweka mwelekeo na kupanga Seria ya Elimu; lazima yabakikishe kuwa vyuo vya kufundisha walimu ni vizuri na, kwa kadiri inavyowezekana, vina tosha. Na lazima yafuatilie na kuelekeza elimu inayotolewakila mahalikatika nchi yetu kubwa hii. Lakini baada ya kuzingatia umuhimu huonila zima walimu wa kuu wa shule zetu na vyuo vyetu wawe na uhuru wa kutosha kabisa kuwa elinisha vijana wetu, wakitumia juhudzi za wananchi wa huko huko sbule zetu ziliko.

Maana yake ni kwamba madaraka ya uendeshaji lazima yagawanywe. Viongozi wetu wa elimu wasijazane mno Dar es Salaam. Makao Makuu yanahitaaji watu wa lazima tu wa kufanya kazi ambazo kweli ni za Makao Makuu. Watu wengine wenye elimu ya juu na vyeo vikubwa la zima wapewe kazi ya kusimamia elimu Mikoani na Wilaya ni, na la zima wapewe madaraka ya kufanya uamuzi katika mambo ya utawala na nidhamu bila kulazimika kuuliza uliza kila kitu Dar es Salaam. Walimu wakuu katika shule za Msingi na za Sekondari vile vile lazima wawe na madaraka ya kweli; hawa si watoto wadogo wala si makarani; ni wa tu wazima, na wataakamu wa elimu walio teuliwa, na arubao wamepati mafunzo ya ziada katika uendeshaji na malengo ya taratibu zetu za elimu. Tunapowanyima madaraka kutosha kwa kweli tunawanyima uwezo wa kuongoza elimu Mikoani, Wilaya ni, Vyuoni, na Shuledi.

Kugawa madaraka kwa dhati ni pamoja na kuwapa madaraka ya kutumia fedha zilizotengwa kwa sababu mbali mbali. Madaraka hayo yakiwapo, basi Walimu Wakuu, na Maofisaelimu wa Mikoani wa Wilaya, wana weza ku wajibika kwa maendeleo, kiwango na manufaa ya elimu katika

maeneo wanayoyatawala. Maana hapo ndipo watakapo-weza kuwa na nafasi ya kutoa huduma bora zaidi na kwa haraka zaidi kwa wanafunzi na kwa walimu. Na inaweze-ka na tukasikia malalamiko machache zaidi ya utovu wa ni dhamu katika baadhi ya shule au ya ukosefu wa walimu katika madarasa yao. Wakati mwingine mambo haya ya natokea, au tuseme yanaendelea, kwa saba du watu wa pale wanaoyatambua makosa hayo hawawezi kuwasikia kwa haraka wale wenye jukuhmu la kuamua.

Maa na tunarudia pale pale kwenye umuhimu wa jukumu la walimu na Walimu Wakuu. Haifai hata kidogo k upuuza umuhimu wao katika vijiji vyetu, katika miji yetu na katika taifa letu. Hatuwezi kuwatuza kwa misahara mizuri au kwa hali nzuri za kazi na za maisha; basi angala u tuwape heshma imayolingana na umuhimu wa oka tika maisha yetu na ya taifa letu.

Lakini kwa kweli kila mwali mu huji jengea heshma yake, na heshma ya kazi ya ualimu. Kama mwali mu ana jiheshimu, ana ni dhamu, na ana jitolea kwa ma nusaa na maendeleo ya wanafunzi na ya jamii, bila shaka atapata heshi ma yake katika jamii. Naa minni kwamba kipimo hiki kinao-nycsha kwamba walimu wetu walio wengi wana zikabili vema kazi tunazowaka bidhi. Tatizo limekuwa kwamba serikali imekuwa ikizungumza juu ya Elimu ya Kuji tegemea, lakini wakati huo huo kuwataka walimu kufuata taratibu zinazoelekezwa kuhudumia jamii ambayo haipo, na wala haitakuwapo. Zaidi ya hapo, tumejaribu kusimamia na kueudesha elimu ya namna hiyo tukiwa na rasilimali haba, tukifuata mfumo mmoja uliotayarishwa na ofisi moja ku bwa, iliyio mahali pamoja.

Sasa na tukabiliane na hali halisi ya Tanzania, na ya mahitaji halisi ya Watananmia. Semina hii ni nafasi ya kujikosoa, na kutokana na kujikosoa huko tupate mareke-bisho. Katika mambo ya elimu tumefanya vizuri, lakini hatukufanya yote ambayo tungeweza na tungepaswa kufanya. Nangojea kwa hamu kupata ripoti kamili ya Semina yenu, na maamuzi ya kujisahihisha ambayo na tumaini yatatokana na semina hii.